# HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANUNUZI TAREHE 29/9/2021

### 1.0 WALIOHUDHURIA

### 1.1 WAJUMBE

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bibi. Elde Kimaro | - | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | - | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Sosthenes Chacha | - | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi | - | Katibu |
| 3. | Bibi. Herieth Makombe | - | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii | - | Mjumbe |
| 4. | Bw. Gwamaka Mwabulambo | - | Mkuu wa Idara ya Afya | - | Mjumbe |
| 5. | Bibi. Delphina Wambura | - | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | - | Mjumbe |
| 6. | Bw. Ally Hatibu | - | Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazingira | - | Mjumbe |

### 1.2 WAALIKWA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Josephat J. Bachubila | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria na Usalama |
| 2. | Bibi. Glory Kessy | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 3. | Bw. Charles Mkwidu | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |

### 1.3 SEKRETARIETI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bibi. Juliana Zacharia | - | Mwandishi wa Mikutano |
| 2. | Bibi. Martha Magaga | - | Afisa Ugavi (PMU) |
| 3. | Bib. Jacquline Flavian | - | Afisa Ugavi (PMU) |
| 4. | Bw. Joshua Mwasimba | - | Afisa Ugavi (PMU) |
| 5. | Bibi. Bahati Mshirazi | - | Afisa Ugavi (PMU) |
| 6. | Bw. Twahir Makwega | - | Afisa Ugavi (PMU) |

### 2.0 MUHT. NA. TEM/ZB/1/9/2021: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 6.00 mchana.

### 3.0 MUHT. NA. TEM/ZB/2/9/2021: KUTHIBITISHA AGENDA

Katibu aliwasilisha agenda zifuatazo kwenye kikao

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda za kikao
3. Kusoma na kuthibitisha mihtasari ya vikao vya tarehe 25/5/2021 na tarehe 29/6/2021.
4. Kuomba idhini ya Kutangaza na kupitisha Kablasha la Zabuni kwa ajili ya ununuzi wa madawati 9584 kwa ajili ya mapokezi ya Kidato cha Kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Kidato cha Tano.
5. Kuomba idhini ya kutangaza na kupitisha kablasha la zabuni ya kukusanya ushuru wa vyoo vilivyopo kwenye masoko ya Manispaa ya Temeke vyoo hivyo ni Temeke Sterio 1, Temeke Sterio 2, Tandika, TAZARA Veterinari, Mbagala Kampochea na Mwembeyanga.
6. Kuomba idhini ya kutangaza kwa njia ya "force account" na kupitisha kablasha la zabuni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 75 ya shule za Sekondari Charnazi (2), Mbagala Kuu (4), Miburani (5), Keko (1), Kurasini (10), Relini (2), Diplomasia (4), Malela (2), Toangoma (4), Charambe (2), Karibuni (7), Tandika (3), Mikwambe

(6), Uhamiaji (3), Kichanga (1), Mbande (1), Nzasa (3), Taifa (3), Ndalala (7), Saku (4) na Lumo (1)

7. Kuomba kuongezewa muda wa miezi 3 kwa Wazabuni wa kukusanya ushuru kwenye vyoo vilivyopo Manispaa ya Temeke Mkataba namba LGA/016/2019-20/HQ/NC/01-LOT 1, LGA/016/2019-20/HQ/NC/01-LOT2,LGA/016/2019-20/HQ/ NC /01-LOT 3, LGA/016/2019-20/HQ/NC/01-LOT4, LGA/016/ 2019-20/HQ/NC/01-LOT5,LGA/016/2019-20/HQ/NC/01-LOT6, LGA/016/2019-20/HQ/NC/01-LOT7,LGA/016/2019-20/HQ/ NC /01-LOT8,
8. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
9. Kufunga kikao.

Wajumbe walipokea agenda hizo kwa ajili ya majadiliano.

**4.0 MUHT. NA. TEM/ZB/3/9/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MIHTASARI YA VIKAO VYA TAREHE 25/5/2021 NA TAREHE 29/6/2021**

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipitia na kusoma mihtasari ya vikao vya tarehe 25/5/2021 na 29/6/2021 na kubaini kuwepo makosa yaliyohitaji marekebisho, hivyo wakaagiza mihtasari hiyo ikafanyiwe marekebisho na kuwasilishwa katika kikao kijacho kwa ajili ya kupitia ili waweze kuithibitisha.

**5.0 MUHT. NA. TEM/ZB/4/9/2021: KUOMBA IDHINI YA KUTANGAZA NA KUPITISHA KABLASHA LA ZABUNI KWA AJILI YA UNUNUZI WA MADAWATI 9584 KWA AJILI YA MAPOKEZI YA KIDATO CHA KWANZA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA KIDATO CHA TANO.**

Katibu aliwasilisha maombi ya idhini ya kutangaza na kupitisha kablasha la zabuni kwa ajili ya ununuzi wa madawati 9584 kwa ajili ya mapokezi ya Kidato cha Kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Kidato cha Tano na kueleza kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke inatarajia kupokea wanafunzi 20636 ambao wanatarajiwa kufaulu darasa la saba 2021. Idadi hiyo ya wanafunzi itapelekea kuwa na upungufu wa madawati 9047 yakilinganishwa na madawati 11589 yanayoachwa na wanafunzi wa Kidato cha Nne.

Kutokana na upungufu huo, Idara inaomba kutengenezewa jumla ya madawati 9584 ambayo yatakuwa kwa ajili ya Kidato cha Kwanza 2021 na yatakayobaki 537 ni ya Kidato cha Tano watakaopangwa kwenye Shule ya MIkwambe na Mbagala.

**MJADALA**

Wajumbe Walipokea na kutoa idhini ya Kutangaza kablasha la Zabuni ya ununuzi wa madawati 9584 kwa ajili ya mapokezi ya Kidato cha Kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Kidato cha Tano.

**AZIMIO**
Kikao cha Bodi ya Zabuni kilitoa idhini ya kutangaza na kupitisha Kablasha la Zabuni kwa ajili ya ununuzi wa madawati 9584 kwa ajili ya mapokezi ya Kidato cha Kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Kidato cha Tano.

**6.0 MUHT. NA. TEM/ZB/5/9/2021: KUOMBA IDHINI YA KUTANGAZA NA KUPITISHA KABLASHA LA ZABUNI YA KUKUSANYA USHURU WA VYOO VILIVYOPO KWENYE MASOKO YA MANISPAA YA TEMEKE VYOO HIVYO NI TEMEKE STERIO 1, TEMEKE STERIO 2, TANDIKA, TAZARA VETERINARI, MBAGALA KAMPOCHEA NA MWEMBEYANGA.**
Katibu akiwasilisha taarifa hiyo alieleza kuwa Halmashauri iliingia mikataba ya kukusanya ushuru wa vyoo na wazabuni:-

| S/N | MZABUNI | CHOO |
|---|---|---|
| 1 | Worker General | Temeke Sterio 1 na 2 |
| 2 | Mtasawa Disable | Temeke Sterio 3 |
| 3 | Hokelai General | Tandika, TAZARA na Mbagala Kampochea |
| 4 | David Bazil | Toangoma na Mwembe Yanga |

Mikataba hiyo ilikuwa ya kipindi cha mwaka mmoja kuanzia 1/10/2020 hadi 30/9/2021.

Kwa taarifa hii aliomba idhini ya kutangaza na kupitisha kablasha la Zabuni ya kukusnaya ushuru wa vyoo vilivyopo kwenye masoko ya Manispaa ya Temeke, vyoo hivyo ni Temeke Sterio 1, Temeke Sterio 2, Tandika, TAZARA Veterinari, Mbagala Kampochea na Mwembeyanga

**MJADALA**
Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazingira alieleza kuwa taarifa inaonyesha tarehe 30/9/2021 mkataba wao unaisha na kikao cha tarehe 29/9/2021, ndio taarifa ya maombi inawasilishwa kikaoni, alihoji kuchelewa huko, lakini pia alishauri kuacha kutangaza na kumpa Mzabuni ni bora Halmashauri ikusanye wenyewe, ni vizuri kukusanya wenyewe kwa muda wa miezi 3 au 4, baada ya hapo tathmini ifanyike kama Halmashauri iendelee kukusanya au isiendelee.

Mkuu wa Kitengo cha Sheria na Usalama alipata wasiwasi na muda wa kutangaza zabuni kwa kuwa muda wa mkataba umeshaisha .

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana alieleza kuwa kama Halmashauri imeweza kukusanya mapato yanayotokana na masoko na maendeleo ni mazuri katika ukusanyaji , alishauri mapato yanayotokana na vyoo Halmashauri isimamie na kukusanya yenyewe.

Mhasibu Mapato alieleza kuwa wanaweza kukusanya mapato hayo ingawa kuna maandalizi ambayo yanatakiwa kufanyika ikiwa pamoja na kuajiri vibarua wa kukusanya mapato hayo, hivyo aliomba muda wa kujiandaa kabla ya kuanza kukusanya.

Katibu alieleza kuwa taarifa hiyo itawasilishwa katika Kikao cha Menejimenti waweze kuridhia Halmashauri kukusanya fedha hizo wenyewe na muda wa kujipanga.

Mwenyekiti alieleza kuwa Bodi hairidhii zabuni ya kukusanya ushuru wa vyoo vilivyopo kwenye masoko ya Manispaa ya Temeke kwa kutumia wazabuni Halmashauri ikusanye yenyewe kwa vyoo vyote, na taarifa iwasilishwe kwenye Kikao cha Menejimenti.

**AZIMIO**

i. Bodi ya Zabuni haijaridhia na haijapitisha Kablasha la kutangaza Zabuni ya kukusanya ushuru wa vyoo vilivyopo kwenye masoko vyoo vyote vinavyomilikiwa na Manispaa ya Temeke.

ii. Bodi ya Zabuni iliagiza Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ikusanye yenyewe Ushuru wa Vyoo vyote vinavyomilikiwa na Manispaa na taarifa iwasilishwe kwenye Kikao cha Menejimenti

## 7.0 MUHT. NA. TEM/ZB/6/9/2021: KUOMBA IDHINI YA KUTANGAZA KWA NJIA YA "FORCE ACCOUNT" NA KUPITISHA KABLASHA LA ZABUNI KWA AJILI YA UJENZI WA MADARASA 75 YA SHULE ZA SEKONDARI CHAMAZI (2), MBAGALA KUU (4), MIBURANI (5), KEKO (1), KURASINI (10), RELINI (2), DIPLOMASIA (4), MALELA (2), TOANGOMA (4), CHARAMBE (2), KARIBUNI (7), TANDIKA (3), MIKWAMBE (6), UHAMIAJI (3), KICHANGA (1), MBANDE (1), NZASA (3), TAIFA (3), NDALALA (7), SAKU (4) NA LUMO (1)

Katibu akiwasilisha taarifa hiyo alieleza kuwa wanaomba ridhaa ya kutangaza kwa njia ya "force account" na kupitisha kablasha la zabuni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 75 ya shule za Sekondari Chamazi (2), Mbagala Kuu (4), Miburani (5), Keko (1), Kurasini (10), Relini (2), Diplomasia (4), Malela (2), Toangoma (4), Charambe (2), Karibuni (7), Tandika (3), Mikwambe (6), Uhamiaji (3), Kichanga (1), Mbande (1), Nzasa (3), Taifa (3), Ndalala (7), Saku (4) na Lumo (1).

**MJADALA**

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana alitoa angalizo la kutompatia mtu mmoja kazi nyingi, alisisitiza sana mtu mmoja asipewe kazi nyingi za kufanya katika ujenzi huo.

**AZIMIO**

Kikao cha Bodi ya Zabuni kiliridhia na kupitisha maombi ya idhini ya kutangaza kwa njia ya "force account" na kupitisha kablasha la zabuni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 75 ya shule za Sekondari Chamazi (2), Mbagala Kuu (4), Miburani (5), Keko (1), Kurasini (10), Relini (2), Diplomasia (4), Malela (2), Toangoma (4), Charambe (2), Karibuni (7), Tandika (3), Mikwambe (6), Uhamiaji (3), Kichanga (1), Mbande (1), Nzasa (3), Taifa (3), Ndalala (7), Saku (4) na Lumo (1)

**8.0 MUHT. NA. TEM/ZB/7/9/2021: KUOMBA KUONGEZEWA MUDA WA MIEZI MITATU KWA WAZABUNI WA KUKUSANYA USHURU KWENYE VYOO VILIVYOPO MANISPAA YA TEMEKE MKATABA NAMBA LGA/016/2019-20/HQ/NC/01-LOT1,LGA/016/2019-20/HQ/NC/ 01-LOT2, LGA/016/2019-20/HQ/ NC /01-LOT 3, LGA/016/2019-20/HQ/NC/01-LOT4,LGA/016/2019-20/HQ/NC/ 01-LOT5, LGA/ 016/2019-20/HQ/NC/01-LOT6,LGA/016/2019-20/HQ/NC/01-LOT 7, LGA/016/2019-20/HQ/ NC /01-LOT8,**

Katibu akiwasilisha taarifa hiyo aliomba kuongeza muda wa miezi mitatu (3) kwa Wazabuni wa kukusanya ushuru wa kwenye vyoo vilivyopo Manispaa ya Temeke.

**MJADALA**

Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazingira alieleza kuwa muda wa miezi mitatu ni mingi sana kwa kuwa bodi imeamua mapato hayo yakusanywe na Halmashauri na sio Mzabuni, hivyo alishauri iwe mwezi mmoja.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana alieleza kuwa kwa kuwa Halmashauri inakusanya wenyewe, mwezi mmoja inatosha kwa ajili ya maandalizi.

Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi aliungana na wajumbe kuongeza mwezi mmoja na sio mitatu.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara alieleza kuwa vyoo vingi vya Halmashauri ni chakavu sana na miundombinu yake ni chakavu pia, na wanachokusanya karibu chote kinatumika katika kufanya marekebisho na ukarabati, hivyo ni vema kufanya ukarabati wa vyoo hivyo pia.

Mwenyekiti alieleza kuwa kwa kuwa wamekubaliana mapato yanayotokana na ushuru wa vyoo yakusanye na wataalam kutoka Manispaa, muda wa kuongeza kwa mzabuni uwe mwezi mmoja tu ili wataalam waweze kujipanga hadi tarehe 1/11/2021, Halmashauri ianze kukusanya wenyewe.

**AZIMIO**

i. Kikao cha Bodi ya Zabuni hakikuridhia nyongeza ya muda wa miezi mitatu (3) kwa Wazabuni wa kukusanya ushuru kwenye vyoo vilivyopo Manispaa ya Temeke
ii. Kikao cha Bodi ya Zabuni kiliagiza Idara ya Fedha na Biashara ijiandae kwa muda wa mwezi mmoja hadi tarehe 1/11/2021 ianze kukusanya mapato yanayotokana na ushuru wa kwenye vyoo vyote vilivyopo Manispaa ya Temeke.

**9.0 MUHT. NA. TEM/ZB/8/9/2021: KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti alifunga kikao saa 7.05 mchana.

............................ ............................

**MWENYEKITI** **KATIBU**

**UMETHIBITISHWA**

**TAREHE .....................**